

## Shairi

*Zainab Omar*

Awali ninaanzia, jina lamola jaliya  
nanyi nawasalimia, vipi mnajisikia

Leo tunamkumbuka, mwalimu wetu hakika,  
ni mtu wa kutajika, sifa zake zimeeneya

Ghafula tukasikia, Vienna hapa Austria  
ameiaga dunia, nyoyo zetu zilinywea

Alikua habagui, kukasirika hajui  
Ni nani hamtambui, kwa huzuni tunalia

Nataja ismu yake, Irmi Hanak jina lake  
lughha fani yake, kiswahili kabobea

Tumepata kubwa pigo, taasisi la Afrika pengo  
hakuwa nayo maringo, hadi sasa tunaliya

Huyu niwetu muhibu, Rabbi usimuadhibu  
umuondoshee tabu, kwa njema zake tabia

Ukweli tumeumiya, kwa mazuri mazoweya  
elimu katupatiya, maisha tutatumia

Huyu kweli mfadhili, watoto wake wawili  
inshallah tutawajali, mola tatusaidia

Mola amuwashie taa, imng'ariye miale  
apate ya manufaa, ya salama na upole

Kila tukiomba dua, humuombea milele  
apate yake shufaa, na peponi awe mbele

Tunawaza na kutafakari, ipi la kumfanyia  
ni dua zilonzuri, Irmi twakuombea

Nasisi tuwemakini, sote tuko safarini  
hata turuke angani, mauti tatufikiya

Apa natia tamati, Irmi kawa hayati  
dhahabu siyo kareti, almasi aminiya.